JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALMASHAURI YA MANISPAA SUMBAWANGA

Fax: 0252802163
Simu: 025 -2802163
E-mail: md.sumbawanga@rukwa.go.t

S. L. P 187
sumbawanga

15/03/2017

HOTUBA YA MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI MWAKA 2017

Wizara ya Maji na umwagiliaji kuanzi mwaka 1988 imekuwa ikiadhimisha Wiki ya Maji kila mwaka hapa nchini kwa kuwashirikisha wananchi na wadau wote wa maji.
Maadhimisho haya yanakwenda sambamba na Azimo Na.47/193 la Umoja wa Mataifa kuwa tarehe 22 Machi ya kila mwaka nchi wanachama waadhimishe Siku ya Maji Duniani ambayo pia ni kilele cha Wiki ya Maji Kitaifa.

Madhumuni ya jumla ya Maadhimisho ya Wiki ya Maji ni kutathmini mafanikio na changamoto nakubadilishana uzoefu katika kuboresha utoaji wa huduma ya Maji na usafi wa mazingira .madhumuni hayo ni pamoja na ;

1. Kuelimisha jamii kuhusu Sera ya Maji na majukumu yao katika kuitekeleza ,
2. Kutathmini maendeleo ya Utekelezaji wa Programu ya Maji , haliya huduma ya maji na usafi wa mazingira na kuweka mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma na uhifadhi rasilimali za maji.
3. Kubadilishana mawazo kati ya wadau na watendaji wa sekta ya maji.
4. Kuwafahamisha wananchi kuhusu Mafanikio ya Sekta ya Maji na changamoto zinazotukabili katika utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira .
5. Kuwahamasisha wadau na wananchi kwa ujumla ili washiriki katika kupanga ,kutekeleza na kuendesha miradi ya majisafi na usafi wa mazingira .
6. Kuendelea kujenga mahusiano na wadau, hususani Wahisani na Asasi zisizo za kiserikali kuhusu changamoto zilizopo.
7. Kujenga mshikamano mingoni mwa wadau mbalimbali wa sekta ya Maji na Usafi wa mazingira.

Wakati wa Maadhimisho hayo ambayo huwa kila tarehe 16 hadi 22 Machi, ya kila mwaka shughuli mbalimbali huwa zinafanyika ikiwa ni pamoja na ;
Uhamasishaji wa jamii kuhusu Utekelezaji wa Sera ya Maji ,Usafi na upandaji wa miti katika maeneo ya vyanzo vya Maji na Uwekaji wa Mawe ya Msingi au Uzunduzi wa miradi iliyokamilika.

Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi imefanya uhamasishaji wa Sera ya Maji kwa jamii husika ili iweze kuuendesha na kuutunza mradi wao wenyewe ili uwe bora endelevu hata kwa vizazi vijavyo, kusafisha vyanzo vya maji, kuanzisha vyombo vya maji, kusimamia ufunguzi wa akaunti za mifuko ya maji, kutoa mafunzo kwa kamati za maji juu ya umuhimu wa kuwa na mifuko ya maji na jinsi ya kuendesha miradi ya maji Pia ofisi ya mkurugenzi inatarajia kupanda miti katika maeneo ya vyanzo vya Maji kwa kushirikiana na Wananchi wao wenyewe Kama inavyoonesha kwenye ratiba , Pia Halmashauri inatarajia kuuzindua mradi wa Maji kwenye sherehe za mbio za Mwenge wa Uhuru Tarehe 08/04/2017 na kuukabidhi kwa Wananchi ili waweze kuuendesha na kuutunza wao wenyewe .

Changamoto:

Pamoja na umuhimu wa maji safi na salama kuwa wazi kwa jamii bado bidhaa hii inaendelea kupungua na kuchafuliwa kwa kasi kubwa katika Kijiji chetu cha Mlanda. Ongezeko la mahitaji ya maji linatokana na ongezeko la watu, msukumo wa maendeleo unaotokea katika jamii kama vile kilimo, umwagiliaji, ufugaji n.k. lakini pia uchafuzi wa maji unasababishwa na shughuli za kilimo na unyweshaji maji mifugo kwenye vyanzo vya maji na Kuharibu miundombinu ya maji.

Wananchi kutochangia fedha ya maji kwenye akaunti ili kuweza kufanya matengenezo pale ambapo miundombinu inapoharibika.

Napenda kutoa shukrani zangu kwa wananchi wote waliohudhuria mahali hapa, Diwani wa kata , Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa kijiji na viongozi wote wa kijiji bila kusahau kamati ya maji kwa ujumla katika kujumuika kwenye maandalizi ya wiki ya Maji.

Nawatakia kazi njema.

………………………………

JUSTIN MALISAWA

MEYA WA MANISPAA

SUMBAWANGA